# JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI

**Namba za simu.**

**Ofisi 0282225109**

**Mkuu wa shule 0787401665/0755180620**

**Makamu mkuu wa shule 0754403477**
**Mtaaluma 0765780201**
**Patron 0752472420**
**Mhasibu wa shule 0755108894**

Shule ya Sekondari Kagango,

S.L.P. 62,

**BIHARAMULO**

*Tarehe…………*

***MZAZI/MLEZI WA** ……………………………..................................................*

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI KAGANGO HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO MKOA KAGERA MWAKA …….**

1. Nina furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **tano** katika shule hii mwaka 2026. Kwa niaba ya walimu, wafanyakazi na wanafunzi wa shule hii, nakupa pongezi na kukukaribisha kwa moyo wa kindugu. Shule ya Sekondari Kagango ipo mjini Biharamulo **½ km**. toka stendi kuu ya mabasi. Mji huu wa Biharamulo unafikika kwa barabara majira yote ya mwaka toka sehemu yoyote yaTanzania.Muhula wa masomo unaanza tarehe ...................................... Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shule kuanzia tarehe ....................... na mwisho wa kuripoti ni tarehe ………………..

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia**

**2.1 Sare ya shule** Sare ya shule hii ni:

- Suruali mbili rangi ya **khaki America** zenye linda 2 kila upande,mifuko 2 mbele na 1nyuma na pindo chini (turn-up) zitakazovaliwa wakati wa masomo,suruali zinapatikana shuleni pia ili kuondoa mkanganyiko wa kitambaa na namna ya ushonaji usiozingatia taratibu za shule (Tafadhali zingatia maelekezo vizuri kuondokana na gharama zisizo za lazima kushona sare mara mbili).mashati mawili mikono mifupi yasiyo na ‘flaps’ au urembo wowote na yenye mfuko mmoja upande wa kushoto,weka kitambaa cheusi alama ya **V** kwenye mabega ya kushoto ya shati hizo.viatu vyeusi vyenye kamba jozi mbili visivyo na visigino virefu na wala siyo ‘boots’,soksi rangi yoyote, mkanda mweusi usiyo mpana wala wenye chuma kipana mbele, sweta rangi ya bluu lenye nembo ya shule bila ufito wowote wala urembo wowote (makoti,majaketi au sweta tofauti na lililoelekezwa hayakubaliki shule.

- Masweta yanaweza patikana shuleni. Aidha kutokana na mfanano wa nguo, mwanafunzi anashauriwa kuweka alama ndogo kwenye nguo yake ili kutofautisha na mwingine .
- Suruali mbili nyeusi zitakazovaliwa nje ya saa za masomo,zinaweza kupatikana shuleni pia.
- Nguo za michezo,bukta na t-shirts za rangi ya bluu,bukta iwe na michirizi myeupe pembeni, raba rangi yoyote na tracksuit ya bluu yenye michirizi myeupe pembeni.
- T-shirt rangi ya bluu yenye kola na isiyo na urembo wowote yenye nembo ya shule itakayovaliwa nje ya saa za masomo, zinaweza kupatikana shuleni kwa Tsh 14,000/= nguo zaidi ya hizi hazitakubaliwa wala kuruhusiwa kuvaliwa isipokuwa za michezo muda wa michezo tu. Kuvaa nguo zisizoruhusiwa ni utovu wa nidhamu.

2.2 **Michango muhimu ya shule**.

- Shilingi 65000/= Michango ya uendeshajiwa shule
- Shilingi 5000/= Kwa ajiri ya kitambulisho.
- Shilingi 5000/= fedha ya tahadhari ambayo haitarejeshwa.
- Shilingi 5000/= kwa ajiri ya nembo ya shule.

NB: Kila mwanafunzi aje na **BIMA YA AFYA YA NHIF**, kwa ambae hana au atakosa alipie Tsh 50,400/= kwenye akaunti ya shule iliyoandikwa hapo chini (bima ya afya ni lazima kwa kila mwanafunzi). Shule itaratibu kwa kushirikiana na NHIF mwanafunzi aweze kukatiwa BIMA hiyo. Shule haitagharamia matibabu ya mwanafunzi mgonjwa asiye na BIMA YA AFYA.Tafadhali hakikisha mwanao anapata BIMA kwa faida yake mwenyewe.**BIMA YA AFYA NI LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI**

2.3 Mahitaji **muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:**

i. Ream mbili za karatasi A4 (double A) na mbili za mistari (rulled papers).

ii. Vitabu vya masomo kulingana na tahasusi uliyochaguliwa kwa kuzingatia mtaala ulioboreshwa, zingatia vitabu toka Taasisi ya Elimu Tanzania (T.I.E) ,orodha ya vitabu vya rejea mbalimbali imeambatanishwa, nunua counter books za kutosha kulingana na masomo (zisipungue 8)

iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia (lazima kuja nayo).

iv. Scientific calculator kwa wanafunzi wote wanaosoma HESABU, FIZIKIA, UCHUMI, KEMIA NA JIOGRAFIA

v. Godoro la 2½ X 6, mto na foronya mbili,shuka jozi mbili rangi ya pinki au bluu, blanketi moja, chandarua kimoja cha 2 ½ X 6.

vi. Vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kijiko na kikombe)

vii. Ndoo mbili (1 ya lita 20 na nyingine lita 10) zenye mifuniko, **ISIPOKUWA HGE, EGM na HKL** wao walete ndoo ya chuma lita 20 yenye mfuniko (material aina ya stainless steel/ aluminium)

viii. Jembe1lenye mpini,mfagio wa nje (chelewa)1,mopa/dekio1, soft bloom1na mfagio mgumu wa plastic 1(hard bloom).

ix. Tochi ya betrii/solata,Toilet papers za kutosha kwa matumizi binafsi na Sanduku imara la kutunzia vifaa mwanafunzi

x. Lita tano dawa ya kufanyia usafi wa choo (inapatikana kwa wingi maeneo jirani na shule)

xi. Pesa za matumizi madogo madogo kwa mwanafunzi mwenyewe

xii. Faili moja la kawaida (folder file) na Stappler machine moja ndogo kwa matumizi binafsi ya mwanafunzi mwenyewe.

**NB**. Michango yote ilipwe kupitia akaunti ya shule **Namba 31701200081, NMB**. Jina LA akaunti kagango secondary school ( tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip) pay inslip moja inatosha kuingiza michango yote na aje nayo shuleni aikabidhi wakati wakuripoti,pia kila mwanafunzi anatakiwa kulipa shilingi elfu tano kwenye akaunti hiyo ya shule kwa ajili ya umeme na maji.Isipokuwa fedha ya T-shirt,sweta na suruali italetwa taslimu wakati wa kulipoti shuleni. (Toa copy mbili za pay inslip ya banki na utakabidhi original, hakikisha unabaki na nakala yako ya cheti cha kuzaliwa baada ya kuripoti na uitunze).

## 3. KANUNI ZA SHULE

Ili shule iweze kuendesha shughuli zake za kila siku bila matatizo lazima kuwa na aina Fulani ya utaratibu na kanuni za shule nazo ni kama zifuatazo: -

I. SAREYASHULE:

Kila mwanafunzi atalazimika kuvaa vazi lake rasmi la shule siku zote za masomo,vazi hilo ni lazima liwe safi na livaliwe kwa njia iliyo sahihi na lazima wakati wote liwe limekamilika

II. HESHIMA NA ADABU

Shule ikiwa ni mahali pa malezi ya vijana wa taifa hili wanafunzi wote lazima waoneshe heshima na adabu kwa wakubwa na viongozi wa aina zote bila kujali kama ni walimu au watu wengine iwe shuleni au nje ya shule. Zaidi ya kuonesha heshima kwa wakubwa na viongozi wote, wanafunzi ni lazima wajiheshimu wenyewe kwa wenyewe bila kujali rangi, hali au kidato.

Yafuatayo ni baadhi ya mambo muhimu ya kuzingatia katika suala la heshima kwa wanafunzi:

a) Wakati mwanafunzi anapozungumza na mkubwa au kiongozi ni lazima asimame kwa adabu na awe mtulivu;itakuwa kosa kwa mwanafunzi kuzungumzana kiongozi wa aina yeyote akiwa ameweka mikono mfukoni, anayumbayumba au kuegemea vitu kama vile meza au ukuta.

b) Kama utakuwa umeketi chini na mkubwa au kiongozi anapita karibu yako ni lazima usimame sawa na kuamkia.

c) Ikiwa uko darasani na mwalimu au kiongazi mwingine yeyote anaingia lazima usimame bila makelele na kuamkia,hali kadhalika kiongozi au mwalimu anapotoka darasani wanafunzi lazima wasimame a mkubwa au kiongozi ni lazima asimame kwa adabu na awe mtulivu;itakuwa kosa kwa mwanafunzi kuzungumzana kiongozi wa aina yeyote akiwa ameweka mikono mfukoni, anayumbayumba au kuegemea vitu kama vile meza au ukuta.

d) Kama utakuwa umeketi chini na mkubwa au kiongozi anapita karibu yako ni lazima usimame sawa na kuamkia.

e) Mwanafunzi anapoitwa na kiongozi yeyote,nilazima atembee kwa haraka na ukakamavu. Usingoje kuitwa mara mbili mbili au kufuatwa.

f) Mwanafunzi wa shule hii atatakiwa kuwa mtiifu kwa viongozi wote wawe waalimu au viranja. Hivyo itakuwa kosa kwa mwanafunzi kukataa kutekeleza mambo anayoambiwa na mwalimu au kiranja. Tabia ya kukataa adhabu haitavumiliwa hapa shuleni.

**iii).** *MAHUDHURIO:*

Hapa shuleni tunafanya shughuli zetu zote kwa wakati uliopangwa kwa hiyo kila mwanafunzi ni lazima awahi mahali anapotakiwa siku zote na wakati wote. Zaidi ya kuwahi wanafunzi wote lazima wahudhurie na washiriki katika shughuli zote za shule kama zitakavyopangwa kwenye ratiba. Tabia ya kutohudhuria shule inaweza kusababisha wanafunzi kufutwa shule. Vile vile tabia ya kuchagua masomo ya kuhudhuria au kufanya mitihani mwanafunzi apendayo na kuacha mingine haitavumiliwa.

**iv).** *UTORO*

Mwanafunzia ukisha fika shuleni asubuhi utatakiwa kubaki shuleni mpaka mwisho wa shughuli za siku. Ni kosa kwa mwanafunzi kufika shuleni na kutoweka baada ya muda bila ruksa.Utoro wa mara kwa mara na utoro wa kupita sehemu zisizoruhusiwa katika eneo la shule unaweza kusababisha kufutwa shule.

**v).** *ULEVI:*

Wakati ukiwa mwanafunzi wa shule hii hurusiwi kushiriki katika mambo ya ulevi au aina yo yote ile ya kileo, iwe pombe, bangi au mirungi. Vile vile hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutembea sehemu zinazouza vileo vya aina yoyote kwa wakati wowote.

**vi).** *UGOMVI:*

Ugomvi kwa mwanafunzi ni haramu;iwe hapa shuleni au nje ya shule.

**vii).** *UVUTAJI WASIGARA:*

Mwanafunzi haruhusiwi kuvuta sigara hasa akiwa katika eneo la shule.Sigara kama anasa za aina nyingine zina madhara ya aina mbali mbali.

**viii).** *MALI YA UMMA:*

Vifaa vyote vinavyotumika hapa shuleni ni mali ya umma, na ni wajibu wa kila mwanafunzi kuhakikisha kuwa vifaa vyote vya shule vinatumiwa kwa uangalifu;haviibiwi,kuharibiwaau kuvisambaza kwenye sehemu ambazo siyo mahali pake.

**ix).** *WAKATIWAVIPINDIVYADARASANI*

Wakati wa masomo ikiwa ni pamoja na vipindi vya dini, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa darasani mwao bila kelele au kutembea tembea.Hii inahusika pia na vipindi vya kujisomea. Kupiga kelele au kutembeatembea wakati wa vipindi vya aina hiyo ni kuwanyima wengine haki yao ya kutumia muda waliopewa.

**x).** *VIRANJA*

Viranja wote waliochaguliwa hapa shuleni ni viranja wa shule nzima na wanayo madaraka kamili juu ya kila mwanafunzi bila kujali ni wa darasa gani au eneo gani. Kumdharau au kutomtii ni kuwadharau waalimu waliomkabidhi madaraka, hii ni kwa sababu viranja wanafanyakazi kwa niaba ya waalimu na wanafunzi wote.

**xi).** *WAFANYAKAZI WASIO WAALIMU:*

Wafanyakaziwasiowalimunisehemuyaviongoziwashulenaniwaleziwawanafunzikama walivyo walimu. Hivyo itakuwa kosa kwa wanafunzi kumdharau au kutomtii mfanyakazi ambaye siyo mwalimu. Wote wataheshimika kama viongozi na walezi wa wanafunzi.

**xii).** *USAFI:*

(a) Kila mwanafunzi atahakikisha kuwa mwili wake,mavazi yake,vifaa na sehemu anazotumia vinakuwa safi wakati wote. Iwe mwiko kwa mwanafunzi wa shule hii kutupa ovyo makaratasi na takataka za aina nyingine kama mabaki ya chakula.Tabia ya kuwa na maandishi mwilini au kwenye mavazi haitaruhusiwa.

b) Shule kama mahali pa malezi mema usafi wa ghaibu ni kitu cha lazima sana. Usafi huu utaonekana katika matendo yako,mwenendo wako,lugha yako na tabia yako kwa ujumla.

**xiii).** *KUOA AU KUOLEWA*

Ni marufuku kwa mwanafunzi kuoa au kuolewa wakati akiwa bado mwanafunzi.Iwapo itadhihirika mwanfunzi ameoa au kuolewa basi atafutwa shule mara moja.

**xiv).** *KAZI ZA MIKONO*

Kila mwanafunzi lazima ashiriki katika kazi za mikono.Uzembe,utegeaji na utoro wakati wa kazi za mikono ni haramu kwa mwanafunzi wa shule hii.

xiv)RADIO/VIFAA VYA MUZIKI:

Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia radioa au chombo kingine chochote cha muziki wakati Wa masomo pamoja na simu za mkononi.Wakati ambao siyo wa masomo kutumia radio bwenini, madarasani, maktaba au karibu na eneo la maofisi haitaruhusiwa.

**xv).** *MAOMBI:*

Maombi ya aina zote ya mwanafunzi ni lazima yapitie kwa mwalimu anayehusika kutegemea aina ya shida. kama maombi ya kimasomo ni lazima yapitie kwa mwalimu wa darasa, ofisi ya Mkuu wa Shule na wasaidizi wake hazitamsikiliza mwanafunzi mwenye shida bila kupitisha shida yake kwa mlezi wake anayehusika.

**xvi).** *KUSHIRIKI KWENYE VILABU VYA MICHEZO*

Mwanafunzi wa shule haruhusiwi kushiriki katika kilabu yoyote nje ya timu za shule na UMISETA.

**xvii).** *UHUSIANO:*

Uhusiano wowote ule wa ufisadi kati ya msichana na mvulana hauruhusiwi.

**xviii).** *SILAHA:*

Nimarufukukwamwanafunzikujashuleninaainayeyoteyasilaha aukifaachochotechenye ncha kali kama vile kisu au kifaa kingine cha aina hiyo hatarishi.

**xix)** *MAKOSA YASIYO NA MARUDI*

(a) Wizi

(b) Uasherati na ushoga.

(c) Ubakaji.

(d) Ulevi na utumiaji madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi n.k, mwanafunzi atakayepatikana na makosa hayo hufutwa shule mara moja.

(e) Kupigana au kupiga mwalimu au mwanafunzi mwenzie nje na ndani ya shule.

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

(g) Kudharau Bendera ya Taifa.

(h) Kuoa au Kuolewa.

(i) Kupata mimba au kuharibu mimba nje na ndani ya shule.

(j) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu. (k) Kukataa adhabu kwa makusudi.

**(l)** Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

**(m)**Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 mfululizo.

**(n)** Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu,walezi na jamii kwa ujumla (o) Uvutaji sigara ama utumiaji wa madawa ya kulevya.

(p) Kushiriki matendo ya uharifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sharia ya nchi.

(q) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni na kupanga nyumba.

(r) Kumilki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule. (s) Kufanya jaribio lolote la kujinyonga au kutishia kujiua kama kunywa simu n.k (t) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

(u) Kutofanya au kugoma kufanya mtihani kwa makusudi. Mwanafunzi atakayepatikana na makosa hayayo hufutwa shule mara moja.

NB**.** **MWANAFUNZI MVIVU NA MKOROFI SHULE HAITAMVUMILIA,AIDHA SHULE HAINA UTARATIBU WA CHAKULA MAALUMU (SPECIAL DIET)**

Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa utapeli(wizi kwa njia ya mtandao) Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwapa taarifa kuwa mtoto wa mzazi husika ni mgonjwa na yuko mahututi mzazi atume pesa.

TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE WA NAMNA HII, USITUME CHOCHOTE,KWANZA WASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI. TUMIA NAMBA ZIFUATAZO

Mkuuwashule...0755180620

Makamumkuuwashule...0754403477

Mwalimu wa taaluma... 0765780201

Mwalimuwamalezi...0620430880/0764476815
Mwalimu wa bweni ...................... 0752472420

MENGINEYO:

Mapambo ya aina yeyote hayaruhusiwi.

(i) Shida zote zipitie kwa mwalimu mlezi wa darasa na hatimaye ngazi zingine zifuatwe.

(ii) Kandambili au viatu vya matairi ya gari haviruhusiwi.Vilevile viatu vyenye visigino virefu ni marufuku hapa shuleni.

(iii) Makucha marefu hayaruhusiwi.

(iv) Nywele ndefu haziruhusiwi.

(v) Ndevu na sharafa ni marufuku hapa shuleni.

(vi) Vipuri kama heleni, pete,na mikufu ni marufuku shuleni.

(vii)Utii wa Kengere,ni lazima kwa mwanafunzi kutii wito wa Kengere mara moja bila kusita kwenye eneo la mkusanyiko.

(viii) Ni marufuku kumiliki dawa zisizotolewa na Daktari na kama mwanafunzi anatumia dawa za kudumu au za jadi uongozi wa shule ufahamishwe ili kuona namna bora ya uhifadhi na matumizi ya dawa hizo.Aidha ni marufuku kupeana dawa au kuazimana dawa hovyo hovyo.

Ni marufuku mwanafunzi kujihusisha na michezo yoyote ya kamali (gambling) na ubashiri (betting) akiwa shuleni

FOMU MAALUMU;

Ukiwa umekubali nafasi hii tafadhali jaza kikamilifu fomu hizi;

(i) Fomu ya kukubali nafasi hii.

(ii)Mkataba wa kumsomesha mwanao.

(iii)Fomu ya vipimo vya daktari.

(iv)Uraia wa mwanafunzi na mzazi.

(v)Fomu maalum ya kuzuia umiliki na matumizi ya simu.

Mwisho:

Unakaribishwa tena katika shule ya sekondari Kagango na wakati wote ukiwa hapa itakubidi kusoma kwa bidii,kutii sheria za shule kikamilifu na kushiriki katika mipango ya elimu ya kujitegemea. Karibu shughuli hizi zote utakazo zifanya zitatahiniwa kila siku na kuwa sehemu ya mtihani wako wa mwisho wa kuhitimu kidato cha sita. Hivyo utavuna ulichopanda.

*KARIBU SANA.*

………………………

**MKUUWASHULE.**

Muhimu:Unaporipoti shuleni uje na fomu hii.

**SHULE YA SEKONDARI KAGANGO**
**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**
**SEHEMU YA KWANZA**

**Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi*:***

1. Jina kamili la mwanafunzi…………………………………………………………………....
2. (a)Tareheyakuzaliwa………………………………………………………………………..
b) Kijiji ulichozaliwa…………………………………………………………………...

   c)Taja jina la kitongoji chako……………………………………………………………….

3. (a) Dini……………………………………………………………………………...... (b) Dhehebu…………………………………………………………………………......

4. (a) Ni raia wa nchi ya ……………………………………………………………....
   (b)Kama sio Mtanzania ni Raia wa…………………………………………………………….

5. (a) Darasa ulilomaliza……………………………………………………………….. (b) Shule uliyotoka……………………………………………………………….

6. (a) Jina kamili la Baba/ Mama/ Mlezi………………………………………………..
   (b)Anwani ya Baba/mzazi/Mlezi…………………………………………………………

   (c) Mahali anapoishi……………………………………………………………
   (d) Mtaa huo uko katika kata ya…………………………………………………………

7. a) Unaishi na nani (Taja jina kamili )……………………………………………………
b) Una uhusiano gani na huyo uliyemtaja?……………………………………………

c) Mzazi/Mlezi anafanya kazi gani?……………………………………………………….

d) Anwani yake…………………………………………………………………………..

8. a) Taja jina la Mwenyekiti wa Kitongoji chako……………………………………………
b) Taja jina la Katibu Mtendaji wa Kata yako……………………………………………...
c) Anwani yake…………………………………………………………………………..

**SEHEMU YA PILI**

**UTHIBITISHO WA MZAZI /MLEZI**

Ninathibisha kwamba kadri ya uwezo wangu maelezo aliyoyatoa mwanangu katika karatasi hii yote ni kweli.

Jina na sahihi ya mzazi/mlezi…………………………………………………………...

## SEHEMUYA NNE

**Sehemu hii ijazwe na ofisi ya makamu Mkuu wa shule**.

Muhuri na Sahihi ya Mkuu wa shule.

1. Jina la mwanafunzi…………………………………………………………………………
2. Namba aliyojiunga na shule (ADM.No.)……………………………………………………
3. Kidato cha ……………………………………………………………………………………...
4. Jina la mzazi/mlezi aliyeandikishwa.……………………………………………………..
5. Shule aliyotoka…………………………………………………………………………………

**MKUU WA SHULE**

**HALMASHAURI YA WILAYA BIHARAMULO**

Shule ya Sekondari Kagango,

S.L.P.62

**BIHARAMULO.**

Kumb.Na.KSS/1/1

*Tarehe………………*

Mzazi/Mlezinamwanafunzi,

……………………………..

…………………………….

……………………………

**FOMU YA KUKUBALI**

Mimi ..........................................................................Nakubali kuchukua nafasi

Niliyopewa kidato cha .............................. shule ya Sekondari Kagango.

Ninaahidi kufuata sheria na masharti yote ya shule.

Sahihi ya Mwanafunzi…………………………………Tarehe …………………….. ……….. Mimi

………………………………………… Mzazi wa …………………………………….

nimeyasoma masharti ya mwanangu kujiunga na shule ya sekondari Kagango na ninakubali na kuahidi kwamba mtoto wangu atafuata masharti yote ya shule. Aidha nitahakikisha kuwa mwanangu atamaliza Elimu ya Sekondari la sivyo nitawajibika.

Tarehe………………………Sahihi ya Mzazi/Mlezi ………………………………

# HALMASHAURI YA WILAYA BIHARAMULO

Shule ya Sekondari Kagango,

S.L.P.62

**BIHARAMULO.**

Kumb.Na.KSS/1/1 *Tarehe………………*

**MGANGA MKUU WA WILAYA/KITUO CHA AFYA.**

Kijana ........................................... ……………………amechaguliwa kidato cha **TANO** katika shule ya Sekondari Kagango Mwezi………. kabla hajakubaliwa katika shule hii ili kuendelea na masomo, ni lazima apimwe kwanza.

Tafadhali nijazie sehemu inayohusika hapa chini baada ya kupima.

Asante kwa ushirikino wako.

**MKUUWASHULE**

````````````````````````````````````````````````````````````````````````````````````````````````````````

Mkuu wa shule,

Shule ya Sekondari Kagango,

S.L.P.62,

**BIHARAMULO.**

Nimempima mwanafunzi aliyetajwa hapo juu na kuona kwamba

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
````````````````````````````````````````````````````````````````````````````````````````````````````````

NB: Fomu hii ijazwe na Daktari/Mganga wa serikali

Sahihi…………………………

**MGANGA MKUU WA WILAYA /KITUO CHA AFYA**

# SHULE YA SEKONDARI KAGANGO

## HATI YA MAKUBALIANO KATI YA UONGOZI WA SHULE, MWANAFUNZI PAMOJA NA MZAZI KUHUSU SHERIA YA KUTOMILIKI SIMU MWANAFUNZI ANAPOKUWA SHULENI.

Kutokana na sababu kuwa suala la wanafunzi wa Bweni kumiliki simu wawapo shuleni bado linaendelea na kuendelea kuathiri masomo ya wanafunzi, licha ya kukatazwa na sheria za shule, ikijumuishwa kwenye makosa yasiyo na marudio, sheria No. 7(i). Imekubaliwa kuwa mwanafunzi yeyote atakayekutwa na simu tena kuanzia tarehe 21/05/2014 ataondolewa shuleni na kusubiri maamuzi ya Bodi ya shule. Ambapo itapendekezwa na kamati ya nidhamu kuwa mwanafunzi huyo afutwe shule .

**JINA LA MWANAFUNZI SAHIHI TAREHE**

**……………………………… ………… ……………….**
**……**

**JINA LA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI SAHIHI TAREHE**

**………………………………………………….. ………… …………..**

**JINA LA MWL.WA NIDHAMU SAHIHI TAREHE**

**…………………………………..… ………………**
**……………..**

**JINA LA MKUU WA SHULE SAHIHI TAREHE**

……………………………………. ..………………
………………

ORODHA YA VITABU VYA REJEA MBALIMBALI

Vitabu hivi ni vya rejea mbalimbali vinavyoweza kukuongezea maarifa zaidi sambamba na vitabu toka T.I.E( mtaala ulioboreshwa)

| Na | Somo | JINA LA KITABU |
|---|---|---|
| **1.** | **CHEMISTRY** | 1.Understanding Chemistry for Advanced level<br>2. Physical chemistry by TIE 2024<br>3. Organic chemistry by TIE 2024<br>4 .General and Inorganic chemistry for advanced level secondary schools by TIE 2024 |
| | | 5 .Chand–Volume I &II |
| 2 | **PHYSICS** | 1.Principles of physics for class XI by S.Chand |
| | | 2.Principles of physics for class XII by S.Chand |
| | | 3. Physics for form five (TIE) 2024 |
| | | 4. Physics for form six (TIE) 2024 |
| | | 5.Advanced level physics by Roger Muncaster |
| | | 6.Advanced level physics by Nelkon &Parker |
| 3 | **BIOLOGY** | 1. Biology for Advance secondary schools student’s book five (TIE) - 2024<br>2.Biological science (BS)–D.J.Taylor,N.P.O Green, G.W, Stout |
| | | 3.New understanding Biology |
| | | 4. S. Chand class XI&XII |
| 4 | **ADVANCED MATHEMATICS** | 1.Understanding pure mathematics (A.J.Sadler D.W.S Thorning) |
| | | 2. Advanced Mathematics for form five (TIE) - 2024 |

| | | |
|---|---|---|
| | | 3. Advanced Mathematics for form six (TIE) - 2024 |
| | | 4.S.Chand's Mathematics for class XII Volume I&2 (Dr. Rama |
| | | Verma) |
| | | 5.Mastering ADV math |
| | | 6 .PureAdvancedMathematics1&2(JK BACKHOUSE NEW EDITION) |
| | | 7.Conceptual Advanced Mathematics for Secondary school form V and VI (P.L. MAYOMBYA) |
| | | 8.Advanced level pure mathematics (C.J Trantor) |
| 5 | **HISTORY** | 1. History for secondary school book five (TIE) – 2024<br>2. History for secondary school book six (TIE) – 2024<br>3. African History for advanced level by Ndaw |
| 6 | **GEOGRAPHY** | 1.Practical geography new syllabus (TIE) -2024<br>2. Maseuza physical &practical geography for form five and six |
| | | 3.Physical Geography book five (D.T.Msabila) |
| | | 4.Practical Geography book five (Zisti Kamili) |
| 7 | **ECONOMICS** | 1.Economics for form form 5 and 6 by Ambros |
| | | 2. Economics for form five and six by ali-2025 |
| | | 3.MicroEconomics by TIE- 2024 |
| | | 4.Macroeconomics for form six by TIE -2025 |
| | | 5. Economics 1 & 2 by CHAND |
| 8 | **KISWAHILI** | KISWAHILI 1<br>1. Nadharia ya Lugha kidato cha 5&6– Nyambari Nyangwine |

| | | |
|---|---|---|
| | 2. | Nadharia ya Lugha–Kiswahili1– Masuko.C. Saluhaya |
| | | KISWAHILI 2<br>1. Nadharia ya fasihi kidato cha tano na sita<br>2. Dafina ya lugha - Isimu na nadharia, na mwandishi RIRON S S MATINDE<br>3. Tafsiri na ukalimani.<br>4. Nadharia ya Fasihi , na mwandishi A.J. MASEBO |
| 14 | | |
| | | |

| | | |
|---|---|---|
| | | TAMTHILIA<br>1. Usaliti mjini, na mwandishi IMBUNGA<br>2. Shujaa Mirambo, na mwandishi EMMANUEL MBUNGO<br>3.Mkwawa wa uhehe, na mwandishi M.M.MLOKOZI<br>USHAIRI<br>1. Fumbo linaloelea, na mwandishi NYAMBALI NYANGWINE<br>2. Malenga wa ziwa kuu, na mwandishi WALLAH BIN WALLAH<br>3. Wosia wa baba, na mwandishi AHMED MOHAMED<br>4. Andamo, msatiri safarini, na mwandishi MOHAMED KHELEF<br>RIWAYA<br>1.Dunia uwanja wa fujo, na mwandishi EMPHRASE KEZILAHABI<br>2. Ua la Faraja, na mwandishi W.E.MKUFYA<br>3. Mirathi ya hatari, na mwandishi C.G.MUNG'ONG'O |
| 9 | **BAM** | 1. BASIC APPLIED MATHEMATICS BY TIE- 2024 |
| 10 | **HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI** | Historia ya Tanzania na maadili shule za sekondari kidato cha tano (TIE)- 2024 |
| 12 | **ACADEMIC COMMUNICATION** | Academic communication ( TIE) - 2024 |